## Mfano wa utendaji dhidi ya ukatili, uonevu, uchokozi na ubaguzi wa Elimu ya msingi Mji wa Jyvaskyla

Wanaoshiriki kwenye elimu wana haki ya kuwa na mazingira salama ya kujifunza. (Sheria ya Elimu ya Msingi 29§)

**Kuzuia kulikopangwa kabla na kuingilia kati mapema**

1. Uwekaji mipango na utaratibu
   - Mwalimu mkuu anaongoza kwa kuweka mipango dhidi ya ukatili, uonevu, uchokozi na ubaguzi.
   - Timu inaundwa kwenye kila shule au atateuliwa mtu anayewajibika ambaye ataratibu na kusimamia kazi ya kupambana dhidi ya ukatili, uonevu, uchokozi na ubaguzi kwenye kitengo chake. Mtu anayewajibika ni mjumbe kwenye kikundi cha huduma za masomo cha jamii.
   - Kwenye mpango wa mwaka wa shu anaandikwa mtu anayewajibika kwa kazi ya kupambana dhidi ya ukatili, uonevu, uchokozi na ubaguzi, malengo, utaratibu wa utendaji na makadirio.
   - Kanuni za utaratibu wa shule, maelekezo ya utendaji kazi na mpango wa utendaji sawa na usawa na utendaji dhidi ya ukatili, uonevu, uchokozi na ubaguzi unapitiwa pamoja na mwanafunzi, walezi na wafanyakazi.
   - Kwenye mpango wa thamani sawa na usawa zinaandikwa kanuni za utendaji, jinsi ya kutengeneza na kusimamia mazingira ya kukubaliwa na kuheshimiwa.

2. Kuimarisha jamii
   - Tunafanya mazoezi kwenye hisia, usalama na ujuzi wa mawasiliano kama sehemu ya saa ya mwaka ya kusimamia ustawi ambayo ndani yake kuna hali zote za maisha ya kila siku.
   - Wafanyakazi wanasaidia mahusiano kwenye vikundi na mahusiano ya rika, kutengeneza vikundi na kuzuia upweke.
   - Jamii yote ya shule inasimamia utambuzi wa mahusiano mema na mrejesho chanya na kujenga utamaduni wa kufanya kazi wenye kuthamini uwingi.
   - Wafanyakazi wanashughulikia suala hilo kwenye masomo na wanaandaa siku na wiki za mada pamoja na wanafunz.i
   - Mwanafunzi anakuwa na nafasi kubwa kwenye shughuli za kuimarisha jamii na ustawi na kuzuia ukatili, uonevu, uchokozi na ubaguzi kupitia majukumu mbalimbali.
   - Wafanyakazi wanajenga ushirikiano wa mahusiano na kuaminiana pamoja na wazazi.
   - Kikundi cha jamii cha huduma kwa wanafunzi kinaweka mipango ya ustawi wa jamii na usalama.

3. Jamii ya shule yenye usalama
    - Hakuna aina yoyote ya ukatili inayokubalika. Jamii yote ya shule inaingilia kati kwenye kila tabia isiyofaa kwa utaratibu.
    - Jamii ya shule inaangalia kwa makini tunu na maadili ya jamii na ikihitajika kuzibadili ili kila mwanajamii aone kukubalika na kuthaminiwa jinsi alivyo.
    - Wanafunzi wanaelewa nini maana ya ukatili, uonevu, uchokozi na ubaguzi, wanaweza kuingilia kati na kusema kwa wafanyakazi.
    - Wafanyakazi wanatambua dalili za ishara za mtu aliyefanyiwa ukatili, uonevu, uchokozi na ubaguzi na wanazungumzia suala hilo pamoja na mwanafunzi na mlezi.
    - Wafanyakazi wanapewa mafunzo kuhusu yaliyomo kwenye mfano wa utendaji.

**Kuingilia kati**

- Wakati wote wafanykazi wa shuleni wataingilia kati wakiona au kupata taarifa kuhusu matukio ya ukatili, uonevu, uchokozi na ubaguzi shuleni na kufafanua hali pamoja na wahusika.
- Wafanyakazi kwanza watazungumza na aliyeathirika na hali hiyo na baada yake pamoja na wahusika wengine.
- Mwishoni mwa ufafanuzi kuwapatanisha na kuandika kwenye kumbukumbu za kielektroniki, jinsi gani tutafanya siku zijazo.
- Wafanyakazi watawafahamisha walezi yaliyotokea siku hiyo hiyo.
- Ikiwa hali inashukiwa kuonyesha dalili za kosa la jinai, wafanyakazi wanatoa taarifa ya ulinzi wa watoto ikibidi au taarifa ya kosa la jinai na taarifa ya ulinzi wa watoto (Sheria ya Ulinzi wa Watoto 25 §). Kwa ujumla ni vizuri kufafanua uhitaji wa msaada kwaa wahusika wote. Ikihitajika wanaweza kushauriana na polisi wa Ankkuri, makadirio ya uhitaji wa huduma kwa familia zenye watoto au ofisi ya upatanisho ya Kati-Finland.
- Ikiwa hali inaendelea watakutana pamoja walezi, wanafunzi, watu wanaowajibika na wafanyakazi wengine wanaohitajika.
- Wafanyakazi wanatoa taarifakwa walezi kuhusu ukatili, uonevu, uchokozi au ubaguzi unaotokea wakati wa safari za shuleni na wanatoa ikihitajika msaada wa kufafanua hali hiyo.

**Kipindi cha ufuatiliaji na msaada wa baadaye**

- Wafanyakazi wanafuatilia hali hiyo mara kwa mara kwa muda mrefu wa kutosha na wanahakikisha uzoefu wa mwanafunzi shuleni na kwenye safari za shule: Kwa mwezi wa kwanza kila wiki, kwa mwezi unaofuata kila baada ya wiki mbili na baada ya hapo kulingana na uhitaji.
- Anayewajibika na ufuatiliaji ni mwalimu wa darasa, msimamizi wa darasa an mtu anayewajibika, ikiwa haikukubaliwa vingine.

- Wafanyakazi wanakadiria uhitaji wa msaada kwa wahusika wote na kikundi. Hatua za misaada binafsi na kwa jamii tunakubaliana kulingana na hali pamoja na wataalamu wa huduma za masomo.
- Wafanyakazi wanawafahamisha walezi kuhusu ufuatiliaji na wanawaongoza wahusika kulingana na uhitaji kwenye huduma za msaada kutoka nje ya shule, kama kazi za Ankkuri, kikundi cha mahusiano ya rika cha wahanga cha MLL au tukipysäkki ya kituo cha kifamilia.
- Ikihitajika mwanafunzi anaandaliwa mazungumzo kuhusu malezi au anaamriwa kwenye shughuli za nidhamu kwa kuzingatia umri wa mwanafunzi, kiwango chake cha maendeleo na mazingira ya tendo na matokeo yake.
- Kazi hiyo inakadiriwa na kuendelezwa kila mwaka kwa misingi ya taarifa zilizokusanywa kwa mfano kwenye maswali ya Afya ya shuleni, maswali ya mwanafunzi na kuridhika na masomo, TEAviisari.